

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MOROGORO**

SHULE YA SEKONDARI KIBOGWA,
S.L.P. 6727,
MOB: 0784 981 617
15/12/2020.

KUMB.NA.

Jina la mwanafunzi

.....

S.L.P. 1880,
MOROGORO.

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIBOGWA WILAYA YA
MOROGORO MKOA WA MOROGORO MWAKA 2021**

1.0 Utangulizi:

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na **kidato cha kwanza** katika shule ya **Kibogwa sekondari** kwa mwaka **2021**.

Shule ya Sekondari **Kibogwa** ipo umbali wa **km 34** kutoka Makao makuu ya Wilaya Mvuha. Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **11/01/2021** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021**. Na mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/01/2021** ndani ya siku saba.

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 Sare za Shule

(a) Sare ya shule hii ni **Shati jeupe mikono mifupi na suruali** rangi damu ya mzee kwa wavulana na wasicha **shati jeupe mikono mifupi na sketi** rangi damu ya mzee kwa wasichana. Maelezo ya mshono **rinda box kwa wasichana na suruali yenye marinda mawili kwa wavulana**.

(b) Rangi ya Hijab ifanane na Sare za shule **iwe nyeupe**.

(c) Sare ya michezo kwa shule hii ni T-shirt "blue" kwa wavulana na wasichana

2.2 Daftari ziwe 11 kubwa kalamu za kutosha, Mkebe wa hesabu pamaja na rula.

2.3 Mahitaji mengine ya kibinadamu (kama yapo yatajwe)

- *Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba kwa wote.*
- *Soksi nyeupe kwa wote.*
- *Sketi iwe ndefu ivuke magoti.*
- *Suruali isibane na iwe na "Turn up" chini.*
- *Daftari 11 (Kumi na moja) kwa wote (Counter book).*
- *Mkanda mweusi kwa wavulana.*
- *Sketi mbili (02) na mashati mawili (02) wasichana*
- *Suruali mbili (02) na mashati mawili (02) wavulana.*

3.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

3.1. Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na-25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya Msingi yafuatayo:

- (a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla jambo la lazima.
- (b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
- (c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (Preparation).
- (d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- (e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- (f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
- (g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- (h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.


3.2. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ufukuzwe shule.

- 1. Wizi.
- 2. Uasherati, ubakaji, Ushoga.
- 3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
- 4. Uvutaji bangi.
- 5. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.
- 6. Kupigana na kupiga.
- 7. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.
- 8. Kudharau Bendera ya Taifa.
- 9. Kuo au kuolewa.
- 10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
- 11. Kutoa mimba.
- 12. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- 13. Kukataa adhabu kwa makusudi.

4.0. Mambo mengine muhimu.

Medical Examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hiyo itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara atakapo ripoti shuleni.

“KARIBU SANA KATIKA SHULE HII”



.....
**MKUU WA SHULE
JACKSON U. NDUNGURU**

**THE HEADMASTER
KIBOGWA SEC SCHOOL
P O BOX 6727
MOROGORO**